TANGAZO LA SERIKALI NA. 264 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu, au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine

isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya kimaandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kibanda" maana yake ni jengo au chumba cha biashara;

"kizimba" maana yake ni eneo ndani ya soko linalotumiwa na wafanyabiashara kuuzia bidhaa lenye ukubwa wa mita za mraba nne au zaidi;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"machinjio" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa lengo la kuchinja mifugo;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda maalumu;

"mazao yanayotokana na shughuli za uvuvi" inajumuisha samaki, dagaa, konokono, uduvi, magamba ya samaki na vitu vyote vyenye asili ya samaki;

"meza" maana yake ni meza zinazotumiwa na wauzaji kwa ajili ya kupanga bidhaa mbalimbali;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kadiri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kulingana na viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na

ada au ushuru

mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au wakala kadiri itakavyokuwa, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala kadiri itakavyokuwa na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalumu kuruhusu shughuli za usafirishaji wa bidhaa yoyote kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni imeshindwa kulipa ada au ushuru ndani ya muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri ujumla wa masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1) na baada ya kupata idhini ya mahakama, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na

mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (3) na (4), kabla ya kuuzwa kwa mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

8.-(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala atakayekusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniw

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili

a

kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Katika kutekeleza majukumu yaliyorejewa katika kanuni ndogo ya (1), Afisa Mwidhiniwa atapaswa-

(a) kutoa taarifa kwa umma au mhusika kuhusiana na kusudio la kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kinachohusika angalau masaa ishirini na nne kabla; na

(b) kuzingatia masharti ya Sheria ndogo hii au sheria nyingine yeyote kuhusiana na mamlaka ya kuingia eneo la umma.

Makosa

10. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kikundi cha watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru kadiri itakavyokuwa;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji

wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Adhabu

11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja..

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria T.S Na. 162 ya 2014

13. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ya Mwaka 2014.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1)*

SEHEMU YA KWANZA

1. ADA NA USHURU WA MIFUGO

A. Ada ya Ukaguzi wa Nyama

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha ada kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe mmoja | 1,500/= |
| 2. | Mbuzi mmoja | 1,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Kondoo mmoja | 1,000/= |
| 4. | Nguruwe mmoja | 1,000/= |

B. Ushuru wa Kuuza Mifugo Mnadani

| Namba | Aina ya Mfugo | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 4,000/= |
| 2. | Mbuzi | 2,000/= |
| 3. | Kondoo | 2,000/= |

C. Ushuru wa maeneo maalumu yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya malisho

| Namba | Aina ya Mfugo | Kiwango cha ushuru kwa mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5,000/= kwa Hekta moja |
| 2. | Mbuzi au Kondoo au Nguruwe | 5,000/= kwa Hekta moja |
| 3. | Punda au Farasi au Ngamia | 3,000/= kwa Hekta moja |

2. ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| Namba | Aina ya Kibali | Kiwango cha Ada kwa Mita za Mraba (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha ujenzi kwa ajili ya nyumba ya makazi | 300/= |
| 2. | Kibali cha ujenzi kwa ajili ya nyumba ya makazi na biashara | 400/= |
| 3. | Kibali cha ujenzi kwa ajili ya biashara au kituo cha mafuta kiwanda | 500/= |

3. ADA NA USHURU WA STENDI AU MAEGESHO NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

**A.** Ushuru wa Kuegesha Magari Kituo Kikuu cha Mabasi

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 3,000/= |
| 2. | Basi dogo | 2,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Teksi | 1,000/= |
| 4. | Magari mengineyo yasiyo ya biashara | 500/= |
| 5. | Pikipiki iliyosajiliwa kwa biashara | 500/= |

**B.** Ushuru wa magari maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya maegesho

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari dogo la mizigo au lori lenye uwezo wa kubeba mzigo chini ya tani 7 | 2000/= |
| 2. | Ushuru wa lori tani 7 | 3000/= |
| 3. | Ushuru wa lori lenye uwezo wa kubeba mzigo tani 8 hadi 10 | 5000/= |
| 4. | Ushuru wa lori lenye uwezo wa kubeba mzigo tani 10 na kuendelea | 10,000/= |

**C.** Ushuru wa usajili wa Teksi

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa usajili wa Teksi | 60,000/= kwa mwaka |

4. ADA NA USHURU WA ARDHI

| Namba | Aina ya Maombi | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kubadili matumizi ya ardhi - makazi kuwa biashara | 20,000/= |
| 2. | Kubadili matumizi ya ardhi - biashara kuwa kiwanda | 25,000/= |
| 3. | Uhakiki wa umiliki wa ardhi | 20,000/= |
| 4. | Uthamini | 3% hadi 5% ya thamani ya mali inayothaminiwa |
| 5. | Ada ya maombi ya viwanja | 20,000/= |
| 6. | Ushuru wa mauziano ya ardhi baina ya mtu na mtu, au baina ya Serikali ya kijiji na mtu binafsi. | 5% ya mauzo kwa Halmashauri ya Wilaya |

5. USHURU WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA

A. Mazao ya chakula

| Namba | Aina ya Zao kwa gunia | Kiwango cha Ushuru yanayozidi tani moja (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 1,500/= |

*Tangazo la serikali na. 264 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Maharage | 2,000/= |
| 3. | Muhogo au udaga au makopa | 1,500/= |
| 4. | Karanga zilizobanguliwa | 3,000/= |
| 5. | Karanga zenye maganda | 1,500/= |
| 6. | Mpunga | 1,500/ |
| 7. | Mchele kilo 100. | 2,000/= |
| 8. | Mchele la kilo 50 | 1,000/= |
| 9. | Alizeti | 1,000/= |
| 10. | Mtama au ulezi au uwele | 1,000/= |
| 11. | Njugumawe au kunde au njegere | 2,000/= |
| 12. | Pumba za mahindi au mpunga | 500/= |
| 13. | Mashudu | 1,000/= |
| 14. | Matunda | 1,000/= |
| 15. | Parachichi | 1,000/= |
| 16. | Mkungu wa ndizi | 500/= |

B. Mazao ya Biashara

Mazao yote ya biashara kama Kahawa, Pamba na Tumbaku yatatozwa 3% ya bei ya kununulia

C. Mazao ya Misitu

| Namba | Aina ya zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru kupasua mbao | |
| | (a) Miti ya asili (kila ubao) | 800/= |
| | (b) Miti ya kupandwa (kila ubao) | 300/= |
| 2. | Gunia la mkaa ndani ya Wilaya kila gunia | 2,000/= |
| 3. | Gunia la mkaa nje ya Wilaya kila gunia | 3,000/= |
| 4. | Ushuru wa nguzo au mirunda zenye sentimita 20 kipenyo | 600/= |
| 5. | Ushuru wa gogo lenye sentimita 20 | 1,000/= |
| 6. | Asali kila lita | 200/= |
| 7. | Nta kila Kilogramu | 200/= |
| 8. | Kuni mita moja ya mraba | 1,500/= |
| 9. | Kitanda | 3,000/= |
| 10. | Kochi seti | 5,000/= |
| 11. | Fremu za milango na madirisha | 2,000/= |
| 12 | Topu za milango | 3,000/= |
| 13 | Kabati | 3,000/= |
| 14 | Fito za kujengea mzigo | 500/= |
| 15 | Mabanzi ya miti ya kupanda | 100/= |

*Tangazo la serikali na. 264 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 16 | Mabanzi ya miti ya asili | 200/= |
| 17 | Kiti au stuli | 500/= |
| 18 | Meza | 1,200/= |
| 19 | Dawati | 1,500/= |
| 20 | Mipini ya aina mbalimbali | 200 kila mpini |
| 21 | Ada ya kibali cha kukata mti | 500 kwa kila mti |

## 6. ADA YA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Mali | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba |
| 2. | Kukodi viti | kwa mujibu wa mkataba |
| 3. | Kukodi mitambo | kwa mujibu wa mkataba |
| 4. | Kukodi vifaa vya kieletroniki | kwa mujibu wa mkataba |
| 5. | Lori la kawaida | 1000 kwa kilometa (bila mafuta) |
| 6. | Lori aina ya Tipa | 1000 kwa kilometa (bila mafuta) |
| 7. | Ada ya pango la nyumba za Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba |

## 7. USHURU KWA MAZAO YATOKANAYO NA SHUGHULI ZA UVUVI

Ushuru wa Mizigo ya Samaki

| Namba | Ujazo | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Tenga la Samaki lenye kilo 100 | 2,000/= |
| 2. | Tenga la Samaki lenye kilo 50 | 1,000/= |
| 3. | Gunia la Dagaa lenye kilo 100 | 2,000/= |
| 4. | Gunia la Dagaa lenye kilo 50 | 1,000/= |
| 5. | Mabondo ya samaki kwa kilo | 1,000/= |
| 6. | Lori lenye mzigo wa samaki au dagaa | 30,000/= |
| 7. | Gunia la konokono | 1,000/= |
| 8. | Gunia la uduvi | 1,000/= |
| 9. | Leseni ya ukusanyaji wa mazao ya samaki kwenye mabwawa | 6,000/= |

8. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Madini ya ujenzi | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 20,000/= kwa miezi sita |
| 2. | Kibali cha kufyatua matofali | 20,000/= kwa miezi sita |
| 3. | Ushuru wa madini ya ujenzi | 3,000/= kwa tripu |

9. UKAGUZI WA AFYA NA MAZINGIRA

| Namba | Aina ya Ukaguzi | Kiwango cha Ada kwa miezi sita (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za starehe, baa, vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba za kulala wageni | 5,000/= |
| 2. | Ukaguzi wa wahudumu wa vyakula | 5,000/= |
| 3. | Maduka ya vyakula | 5,000/= |
| 4. | Kiwanda cha kuoka mkate au maandazi | 5,000/= |
| 5. | Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma | 5,000/= |
| 6. | Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara | 10,000/= kila ombi |
| 7. | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 150,000/= kwa mwaka |
| 8. | Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya | 25,000/= kwa kila ombi |
| 9. | Ukaguzi wa viwanda vya kati | 100,000/= kwa mwaka |
| 10 | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 50,000/= kwa mwaka |
| 11 | Ukaguzi wa bucha | 5,000/= kwa mwaka |
| 12 | Ukaguzi wa machinjio | 5,000/= kwa mwaka |
| 13 | Ukaguzi wa saluni | 2,000/= kwa mwaka |
| 14 | Kupima Afya Wahudumu Wa Baa au Hoteli au Migahawa | 3,000/=kwa kila baada ya miezi mitatu |

10. ADA YA SHUGHULI ZA BURUDANI NA TIBA MBADALA

| Namba | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Disko za siku za kawaida au sikukuu na mwisho wa juma | 20,000/= kwa tukio |
| 2. | Waganga wa jadi | 50,000/= kwa mwaka |

*Tangazo la serikali na. 264 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Michezo ya sanaa za maonyesho au ngoma au maigizo au sarakasi au michezo ya nguvu au nyimbo | 5,000/= kwa tukio |
| 4. | Shughuli za sanaa za ufundi au picha au upakaji rangi au vinyago | 10,000/= kwa tukio |
| 5. | Mchezo wa pool table | 10,000/= kwa mwezi |
| 6. | Kuendesha promosheni au matangazo katika bar au hoteli au maeneo ya wazi. | 20,000/= kwa siku |
| 7. | Kuonyesha mpira | 5,000/= kwa mwezi |
| 8. | Utundikaji wa matangazo ya vitambaa | 2,000/= kwa mwezi |
| 9. | Utundikaji wa matangazo ya karatasi | 10,000/= kwa mwezi |
| 10 | Sherehe za harusi au kipaimara na ubatizo katika kumbi za starehe | 10,000/= |

11. USHURU WA MADINI

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Makarasha | 50,000/= kwa mwaka |
| 2. | Mwalo | 50,000/= kwa mwaka |
| 3. | Mchanga | 1,000/= kila mfuko |
| 4. | Ada ya umiliki wa ardhi itakuwa 10% ya uzalishaji, na kama ardhi ni ya kijiji italipwa 10% kwa mgawanyo wa 5% ya kijiji na 5% ya Halmashauri ya Wilaya. | |

12. USHURU WA VIBANDA NA VIZIMBA AU MEZA KATIKA MASOKO NA MAGULIO

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kuzunguka masoko ya Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba |
| 2. | Kuzunguka vituo vya mabasi | kwa mujibu wa mkataba |
| 3. | Ushuru wa vibanda vya mitumba | kwa mujibu wa mkataba |
| 4. | Pango la meza katika masoko ya Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba |
| 5. | Pango la vibanda vya Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Pango la bucha | kwa mujibu wa mkataba |

13. USHURU AU ADA ZA HUDUMA NYINGINE

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ushuru au Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kitu kinachonadiwa mnada | 5% ya bei ya mnada |
| 2. | Choo cha umma | 300/= kila anapoingia |
| 3. | Kuendesha utafiti mambo ya kale na tafiti nyingine zinazofanana na hizo | 50,000/= kwa Raia wa Tanzania na Dolla 70 kwa Raia wa kigeni. |
| 4. | Gari la kusomba mbolea | 1,000/= kwa kila Tani |
| 5. | Kibali cha kutangaza katika sherehe | 30,000/= kwa mwaka |

14. VIWANGO VYA ADA YA TAKA KWA MWEZI

| Namba | Aina ya Huduma | Ada ya Taka kwa Mwezi maeneo ya Biharamulo Mjini (Rukaragata, N'gambo, na Biharamulo Mjini), Lusahunga (Nyakanazi), Kabindi, Nyakahura na eneo jingine litakaloainishwa kwa Azimio la Halmashauri | Maeneo mengine katika kata na vijiji vyote nje ya mji |
|---|---|---|---|
| 1 | Baa au hoteli au Grosari au pabu | 5,000 | 1000 |
| 2 | Bucha | 2000 | 1000 |
| 3 | Nyumba za kuishi kwa kila kaya | 2,000 | 1,000 |
| 4 | Watengenezaji wa juisi au bisi au barafu | 1,000 | 500 |
| 5 | Mgahawa au Baba au Mama lishe | 3,000 | 1,000 |
| 6 | Wachoma chipsi au kuku au nyama | 2000 | 1000 |
| 7 | Zahanati za watu binafsi | 4,000 | 2,000 |
| 8 | Vituo vya afya vya watu binafsi | 5,000 | 3,000 |
| 9 | Hospitali za watu binafsi | 15,000 | 5,000 |
| 10 | Maduka ya dawa muhimu na maduka ya dawa za kilimo | 3,000 | 2,000 |
| 11 | Maduka ya dawa 'Pharmacy" | 5,000 | 2,000 |
| 12 | Vizimba au vioski au meza za biashara | 1,000 | 500 |
| 13 | Mafundi seremala na watengeneza | 5,000 | 2,000 |

*Tangazo la serikali na. 264 (linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | samani | | |
| 14 | Wachomelea vyuma | 5,000 | 2,000 |
| 15 | Karakana, kuranda mbao na kuuza mbao | 5,000 | 2,000 |
| 16 | Shule binafsi na vyuo binafsi | 5,000 | 3,000 |
| 17 | Maduka ya jumla | 2,000 | 1,000 |
| 19 | Maduka ya rejareja | 2,000 | 1,000 |
| 20 | Wauza mkaa | 3,000 | 1,000 |
| 21 | Vilabu/wauza pombe za kienyeji | 1,000 | 500 |
| 22 | Saluni | 2,000 | 1000 |
| 23 | Nyumba za kulala wageni | 5,000 | 3,000 |
| 24 | Maduka ya vitabu au steshenari au internet café | 2,000 | 1,000 |
| 25 | Maduka ya vifaa vya ujenzi | 3,000 | 1,000 |
| 26 | Vituo vya mafuta | 5,000 | 2,000 |
| 27 | Wafyatua tofali za kuuza | 3,000 | 1,000 |
| 28 | Mashine za kusaga na kukoboa nafaka | 3,000 | 2,000 |
| 29 | Ofisi na Taasisi | 5,000 | 3,000 |
| 30 | Wauza mitumba katika vibanda | 2,000 | 500 |
| 31 | Wauza mitumba kwenye soko | 1,000 | 500 |
| 32 | Wauza nafaka | 2,000 | 500 |
| 33 | Eneo la machimbo ya Madini | 2000 | 2000 |
| 34 | Mafundi pikipki | 2000 | 1000 |
| 35 | Mafundi baiskeli | 1000 | 500 |
| 36 | Waziba pancha mitaani | 1,500 | 500 |
| 37 | Wafugaji kuku au ndege wengine kuanzia 10 | 1,000 | 500 |
| 38 | Wafugaji wa Ng'ombe na Wanyama wengine zaidi ya 10 | 3,000 | 1000 |
| 39 | Gereji/ fundi magari | 3,000 | 1,000 |
| 40 | Magari madogo yanayoshusha mizigo kwenye masoko tani 1hadi 7 | 3,000 | 1,000 |
| 41 | Magari makubwa yanayoshusha mizigo kwenye masoko yenye uwezo wa kubeba tani 8 na kuendelea | 5,000 | 2,000 |
| 42 | Magari madogo tani 1 hadi 7 yanayoshusha mizigo maeneo mengine nje ya eneo la soko magari | 3,000 | 1,000 |
| 43 | Magari madogo tani 8 na kuendelea yanayoshusha mizigo maeneo mengine nje ya eneo la soko | 5,000 | 2,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi…………...…. mwaka ………...… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ……………ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe …………………..ya mwezi …………… mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: …………………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

*Tangazo la serikali na. 264 (linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya wilaya ya Biharamulo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya wilaya Biharamulo kilichofanyika Tarehe 26 mwezi, Agasti, 2022

INNOCENT MBANDWA MUKANDALA
*Mkurugenzi Mtendaji (w)*
*Halmashauri ya Wilaya Biharamulo*

LEO MATHEW LUSHAHU
*mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Biharamulo*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
30 Novemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*